

KUKAKAMAA KWA WAJIPATIAJI WA LUGHA YA KISWAHILI KAMA LUGHA YA PILI:
MIFANO KUTOKA KWA JAMII YA WAKINGA

Arnold B.G.Msigwa
Taasisi ya Taaluma za Kiswahili
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
gawasike@udsm.ac.tz

Ikisiri

Wajipatiji wa lugha ya Pili hukabiliwa na changamoto mbalimbali katika mchakato wa ujipatiaji wa lugha hiyo. Chanzo cha changamoto hizo zinaelekea kutokuwa na namna moja ya kuzieleza. Makala hii kwa hiyo, inalenga kufafanua chanzo cha kukakamaa kwa wajipatiji wa lugha ya pili katika jamii ya Wakinga. Swali linaloibuliwa na makala hii ni, Je, kukakamaa kwa wajipatiji wa Lugha ya Kiswahili katika jamii ya Wakinga kunasababishwa na nini?